**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA `SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI**
**SHULE YA SEKONDARI MAFISA**
**S. L. P. 24 – SONGE – KILINDI**

**Kumb. Na. KDC/MFS/ADM/01/16**

Jina la Mwanafunzi:_______________________________________________
S. L. P.________________________________________________________

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAFISA WILAYA YA KILINDI MKOA WA TANGA MWAKA, 2021.**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Mafisa inakupongeza kwa kupata nafasi hii. Ni matumaini ya Shule na Taifa kwa ujumla kwamba utatumia nafasi hii vizuri. Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe 6/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

**a) Wavulana;**

i. Suruali rangi ya damu ya Mzee isiyo na mapambo yoyote zaidi ya **RINDA** mbili za mbele, mfuko mmoja wa nyuma na mifuko miwili pembeni. Pia isiwe ya kubana mwili.
ii. Mashati mawili yenye mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto na yasiwe ya kubana mwili.
iii. T- shirt za sare ya Shule kwa Tshs 12,000 /= na Tshs 3,000 ya nembo ya Shule
iv. Viatu vyeusi vya ngozi (jozi mbili) visivyo na visigino virefu na viwe vya kufunga kwa kamba na soksi nyeusi jozi mbili.
v. Sweta ya rangi ya bluu

**b) Wasichana;**

i. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto na yasibane mwili
ii. Sketi mbili rangi ya damu ya mzee mshono wa **RINDA BOX** na ziwe ndefu za heshima na zisibane mwili.
**AU**
Suruali kitambaa kizito rangi ya damu ya mzee iwe ndefu na pana na shati yake nyeupe ndefu (nusu kanzu) yenye mipasuo pembeni na yenye mikono mirefu.
iii. T – Shirt za sare ya Shule kwa Tshs. 12,000/= zinapatikana Shuleni na Tshs 3000 ya nembo ya shule.
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kufunga kwa kamba na soksi nyeupe jozi mbili.
v. Sweta rangi ya bluu

**MUHIMU:** Rangi ya hijabu ifanane na sare za Shule na ishonwe kukidhi malengo ya hadhi ya vazi hilo na si vinginevyo. Hijabu isiwe kubwa iwe ya wastani

**VIFAA VYA MICHEZO;**

Sare za michezo kwa Wanafunzi wote zitakuwa ni

i. Track suti za bluu/ nyeusi
ii. T – Shirt ya bluu/ njano isiyo na maandishi yoyote
iii. Viatu vya michezo, Raba nyepesi

**VIFAA VYA USAFI;**

Kila Mwanafunzi aje na ufagio mmoja wa chelewa

**CHAKULA;**

Kwa ajili ya chakula cha mchana kwa muhura kila Mwanafunzi anatakiwa aje na

i. Tshs 10,000/= kwa ajili ya mpishi na viungo
ii. Maharagwe Kg 10
iii. Mahindi Kg 24

**VIFAA VYA DARASANI;**

i. Aina ya counter book 10 isiyopungua Quare 2
ii. Begi la Shule na siyo Rambo wala mfuko mwingine wowote
iii. Dictionary (Kamusi ya kiingereza)
iv. Mathematical set (mkebe wa mahesabu), Rular ndefu pamoja na kalamu ya mkaa (PENSELI) aina ya HB

**PAMOJA NA BARUA HII NAAMBATANISHA NAKALA YA:**

i. Sheria za Shule (**ZISOME UZIELEWE**)
ii. **MEDICAL EXAMINATION FORM** (Fomu ya taarifa ya Afya): Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali na kukabidhiwa kwa mkuu wa Shule siku ya kuripoti.
iii. Fomu ya kukiri kwa mzazi na Mwanafunzi, ijazwe kukamilifu na kukabidhiwa kwa MKUU wa Shule siku ya kuripoti.
iv. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa/ **AFIDAVIT**

**KARIBU SANA MAFISA SEKONDARI**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI

**CHARLES MGOMBA**
**MKUU WA SHULE**
**0686-767617**

## 1. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII NI:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayoletwa na Wizara yenye dhamana nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya Msingi yafuatayo ambayo ndio sheria na kanuni muhimu ukiwa hapa Shuleni.

a) Heshima kwa Viongozi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani ya Shule ni muhimu.

c) Kutimiza na kuhudhuria kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).

d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa.

e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule.

f) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa Wanafunzi wako katika Shule.

g) Kuzingatia ratiba za Shule wakati wote.

## 2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAKFUKUZWA SHULE

a) Wizi.

b) Uasherati na ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi, kubeli n.k.

e) Kupigana na kupiga.

f) Kudharau Bendera ya Taifa.

g) Kuoa au kuolewa.

h) Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na je ya Shule.

i) Kutoa mimba.

j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa Shule au watu.

k) Kukataa adhabu kwa makusudi.

l) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI**
**SHULE YA SEKONDARI MAFISA**
**FORM YA MAELEKEZO**

---

**SEHEMU "A" KUKUBALI KUJIUNGA (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

Mimi_______________________________________________________nakubali kuipokea nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari___________________________ na ninaahidi kuitumia nafasi hiyo vizuri. Pia naahidi kutekeleza maagizo na kufuata taratibu na sheria za Shule.

**Sahihi ya Mwanafunzi**_____________________________**Tarehe**___________________________

**SEHEMU "B" MKATABA WA KUTOGOMA, KUTOFANYA VURUGU SHULENI (IJAZWE NA MWANAFUNZI)**

Mimi_______________________________________________________naelewa kuwa kufanya mgomo au vurugu Shuleni ni kosa la jinai. Hivyo naahidi kutoshiriki katika mgomo au kufanya fujo yoyote hapa Shuleni. Kama kuna jambo lolote litakalotakiwa kuchangia hoja nitafuata taratibu zote za kistaarabu zilizowekwa.

Sahihi ya Mwanafunzi______________________________Tarehe___________________________

**SEHEMU "C" MAELEZO YA MZAZI/ MLEZI (IJAZWE NA MZAZI/ MLEZI)**

Mimi_______________________________________________________AMBAYE NI Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi____________________________nakubali nafasi aliyopewa mwanangu kuendelea na masomo. Na nimezisoma na kuzielewa sheria za Shule. Naahidi kumsaidia mwanangu kulipa michango yote na mahitaji muhimu ya Mwanafunzi katika fomu ya kujiunga. Nitasaidia Shule katika malezi ya mwanangu.

**Sahihi ya Mzazi/ Mlezi**_____________________________**Tarehe**___________________________

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**To Medical Officer**

______________________________

______________________________

Mr/Miss ______________________________

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for a full time student. The examination should be as indicated below. In each category or sub category of which will render a girl student ineligible for studies.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAFISA

Date 15/12/2020 Signature ______________

**MEDICAL CERTIFICATE**
**(To be completed by Government medical Officer)**

I have examined the above named and consider that he/ she is physical fit/ unfit and mentally fit/unfit for a fulltime student

1) A. Eyesight ______________________________
   B. Hearing ______________________________
   C. Speech ______________________________
   D. Limbs ______________________________
   E. Venereal disease ______________________________
   F. Leprosy ______________________________

2) Neuroses ______________________________

3) Other Serious disease ______________________________
______________________________

4) Pregnancy ______________________________

Station ______________________ Signature ______________________

Date ______________________ Designation ______________________